# WILAYA YA KIRINYAGA

# DARASA LA NNE MUHULA WA TATU

PENPLUS KIRINYAGA

# KISWAHILI

**Muda: Saa 1 dak 40**

***Soma kifungu hiki na ujaze mapengo 1-15 kwa majibu yanayofaa:-***

__1___ asubuhi na mapema. Siku __2_ tulikuwa tukienda sokoni kunua vitu. Soko__3___ lilikuwa kubwa sana. Tuliingia garini na kulipa__4 ___ ya kusafiria. Mikononi tulibeba vyondo vya _5 bidhaa zetu. Dereva__6___ gari nalo __7__ na kung'oa __8__ huku likiacha wingu la moshi nyuma. Tulifika sokoni salama__9___.Wauzaji waliwakaribisha __10___ wao kwa heshima na kuwahimiza wanunue kwa wingi.

Sisi __11___ tulinunua nafaka na matunda.Tunda __12___ lilikuwa kubwa mpaka likawashangaza watu wote. Tulimaliza pesa __13__ mpaka ikatulazimu kurudi __14-_ miguu.Safari ilikuwa __15___ lakini tulifaulu.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. Tulidemka | B. Tulirauka | C. Tulirudi | D. Tulikuja |
| 2. | A. hio | B. hilo | C. hiyo | D. hii |
| 3. | A. hii | B. hili | C. hizo | D. hilo |
| 4. | A. dereva | B. pesa | C. nauli | D. kitu |
| 5. | A. kubebea | B. kubeba | C. kupepa | D. kupepea |
| 6. | A. aliuwakisha | B. aliwasha | C. aliwakisha | D. likakuruma |
| 7. | A. liliguruma | B. likanguruma | C. likaguruma | D. likakuruma |
| 8. | A. nanga | B. kamba | C. magurudumu | D. safari |
| 9. | A.salmini | B.salmini | C. salimini | D. salaumuni |
| 10. | A. wauzaji | B. wenyeji | C. wageni | D. wateja |
| 11. | A. wote | B. sote | C. zote | D. nyote |
| 12. | A. lingine | B. ingine | C. jingine | D. mengine |
| 13. | A .zote | B. yote | C. lote | D. kote |
| 14. | A. ya | B. wa | C. na | D. kwa |
| 15. | A mrefu | B. ndefu | C. refu | D. kurefu |

***Fuata maagizo kujibu maswali nambari 16-30 kwa usahihi***

16. Nikimsalimu mjomba "shikamoo mjomba" atajibu____
    - A. marahaba mjomba
    - B. sina neno
    - C. shikamoo pia
    - D. marahaba mpwa

17. Andika wingi wa sentensi ifuatayo
    Nguo yangu inavutia
    - A. Nguo zangu zinavutia
    - B. Nguo zetu zinavutia
    - C. Nguo zenu zinavutia
    - D. Nguo yenu inavutia

18. Kamilisha sentensi ifuatayo kwa usahihi
    Chakula ____ kina viungo huwa kitamu.
    - A. chenye
    - B. ambacho
    - C. yenye
    - D. ambako

19. Katika bendera yetu ya Kenya, ni rangi gani inayopatikana katika sehemu ya juu zaidi?

A. Nyeusi

B. Nyeupe

C. Nyekundu

D. Kijani

20. <u>Tumia kiashiria sahihi kukamilisha sentensi hii</u>

Viatu ___ vinapendeza.

A. vyako B. yako

C. hivi D. vyote

21. Kiungo cha mwili kinachosafisha damu huitwa___

A. moyo B. pafu

C. figo D. ini

22. Neno 'pua' lipo katika ngeli gani?

A. U-ZI B. I-ZI


C. LI-YA D. U-YA

23. Vazi la wanawake ambalo hushikilia maziwa huitwaje?

A. Kanchiri B. Shimizi

C. Gauni D.Gagro

24. Umbo hili huitwa___



A. mche mstatili B.mraba

C. mche mraba D. mstatili

25. Mnyama wa porini anayefanana na ng'ombe anaitwa___

A.pundamilia

B. twiga

C. swara

D.mbogo

26. Andika kinyume cha 'mfalme'

A. Mkurugenzi

B. Malkia

C. Mwanamwali

D. Binti

27. <u>Kanusha :</u>

Sisi hula asubuhi

A. Sisi hatukuli asubuhi

B. Sisi hatulangi asubuhi

C. Sisi hatuli asubuhi

D. Sisi hukula asubuhi

28. Sehemu ya nyuma katika mguu huitwa___

A. kisogo

B. utosi

C.kisigino

D.kisugudi

29. Chagua neno lililoandikwa kwa usahihi kumaanisha 'Gari la mizigo'

A. Mgongoteni

B. Mkongoteni

C. Mwokongoteni

D. Mkokoteni

30. Kombe ni makao ya kiumbe kipi?

A. Buibui B. Kobe

C. Nyuki D. Konokono

***<u>Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali 31-40</u>***

Darasa letu liliteuliwa kwenda kwa ziara ya mkoa wa Bonde la Ufa.Tulikuwa na bashasha. Kwa wengi wetu ilikuwa ni mara ya kwanza kuzuru mkoa huo. Usiku uliotangulia siku ya safari sikulala. Nilipata usingizi wa manga'munga'mu. Usiku ulikuwa mrefu. Siku iliyofuata nilidamka alfajiri. Nilioga kwa maji vuvuwaa. Nilivaa na kula kiamsha kinywa.

Nilitoka nyumbani na kwenda masia hadi shuleni. Wanafunzi wengine tayari walikuwa wamewasili kila mmoja wetu alikuwa na matumaini makuu. Hatukujua njia ya usafiri kwa sababu kama shule nyingine katika maeneo yale, shule yetu haikuwa na basi.Tulipiga gumzo tukisubiri. Muda si muda, basi moja la kampuni ya usafiri wa umma liliwasili. Tulipiga makofi ungedhani ni mgeni wa heshima aliyewasili. Ilikuwa pia ni mara yangu ya kwanza kuabiri basi kubwa kama hilo.

Tuliitwa majina na kuingia basini mmoja mmoja. Tulikuwa wanafunzi arubaini na wanane. Tuliaandamana na walimu sita. Utingo naye alikuwa tayari kutuelekeza kuhusu sheria za basi lile. Alisisitiza kuwa sharti kila mwanafunzi afunge ukanda wa usalama. Shanta zetu ziliwekwa kwenye karia. Baada ya maombi mafupi, safari iling'oa nanga. Basi lilienda kwa mwendo wa kadiri. Jambo hilo lilitusaidia kuona mandhari ya nchi. Tuliwasili Nakuru mwendo wa saa saba baada ya kusafiri kwa saa nne. Tulipelekwa kwenye hoteli tulikojionea vituko. Vyoo vya kufyatua vilikuwa maajabu yaliyuotuacha tumeduwaa.

Asubuhi iliyofuata, tulienda kwenye kasoko ka Menengai na kumqlizia siku kwenye mbuga ya wanyama ya ziwa Nakuru. Huko tuliona heroe, manyani, nyati na twiga. Turirudi tukiwa wachovu na kulala fofofo. Tuliamshwa siku iliyofuata na kuenda moja kwa moja hadi Ziwa Bogoria. Hapo kuna upeo wa maajabu. Maji yanayochemka hutoka ardhini. Tulirudi Nakuru tukiwa na hadithi tele za kusimulia. Siku ya mwisho tulifunga virago vyetu na kurudi nyumbani. Ziara hiyo itadumu kwenye kumbukumbu zetu.

31. Kwa nini msemaji alikuwa na usingizi wa mang'amung'amu?
A. Alikuwa na maradhi yaliyomsumbua
B. Usiku ulikuwa mrefu
C. Alikuwa na hamu ya kusafiri
D. Ilikuwa ni kawaida yake kutolala

32. Usiku unaweza kuwa mrefu ikiwa_____
A umelala mapema
B. hujapata usingizi mzuri
C. umelala usingizi wa pono
D. unaenda safari

33. Ni kweli wanafunzi wale huenda shuleni ___
A. kwa basi
B. kwa baiskeli
C. kwa gari
D. kwa miguu

34. Wanafunzi walisafiri kwa____
A. basi la shule
B. basi la kukodisha
C. baiskeli
D. matatu ya umma

35. Safari hii ilikuwa na jumla ya watu wangapi?
A. Arubaini na nane
B. Hamsini na wanne
C. Hamsini na mbili
D. Hamsini na nne

36. Safari hii iling'oa nanga saa ngapi?
A. Saa saba
B. Saa nne
C. Saa tatu
D. Saa moja

37. Msaidizi wa dereva huitwa____
A. utingo
B. msaidizi
C. mwalimu
D. dereva mdogo

38. Wanafunzi walizuru kasoko ya Menengai ____
A. siku ya tatu
B. siku ya kwanza
C. siku ya nne
D. siku ya pili

39. Ni nini ambacho hakikuwa ndani ya gari?
A. Orodha ya majina
B. Shanta za wanafunzi
C. Usukani
D. Viti vya gari

40. Kilichowashangaza zaidi wanafunzi ni_____
A. vyoo vya kufyatua
B. kasoko ya Menengai
C. maji yanayochemka kutoka ardhini
D. kuona heroe ndani ya maji

***Soma habari kisha ujibu maswali 41-50***

Kuna maradhi ya aina mbalimbali. Yapo yaliyo na dawa na yasiyo na dawa. Kuna ndwele ambazo husambazwa na wadudu na nyingine husababishwa na uchafu. Ugonjwa wa kipindupindu husababishwa na uchafu. Ni ugonjwa ambao unaweza kuua kwa urahisi. Ugonjwa kama ukimwi hauna tiba na unatisha kama zimwi.

Lakini ni ugonjwa upi ambao huwaua watu wengi zaidi barani Afrika? Utafiti unaonyesha kuwa ugonjwa wa malaria ndio unaoua watu wengi zaidi. Ugonjwa huu huenezwa na mbu ambao hufyonza damu ya binadamu. Wakati wa msimu wa masika, watu wengi hupata ugonjwa huu kwa sababu mbu hutaga mayai kwa wingi na viluwiluwi huanguliwa na kukua haraka.

Wasemavyo wahenga, kinga ya shinda tiba. Ugonjwa wa malaria una tiba. Kinachosababisha vifo ni ulegevu wa binadamu. Mgonjwa anapaswa kutafuta huduma za matibabu punde anapougua. Akifanyiwa uchunguzi mapema huweza kutibiwa kwa urahisi bila kulazwa hospitalini. Watu wanapaswa kusafisha mazingira, kukata nyasi na kunyunyuzia mafuta maji yaliyotuama. Wakifanya hivyo mayai hayawezi kuanguliwa. Mbu hawana maisha marefu. Baada ya muda mfupi watakuwa wameisha. Ni vyema watu wajifunike kwa vyandarua wakati wa kulala ili wasiumwe na mbu.

Hali kadhalika, inapendekezwa kuwa ukienda mahali palipo na historia ya malaria ni vyema kumeza vidonge vya kuzuia ugonjwa huu. Ni aibu kama tutaendelea kuangamizwa na maradhi ambayo yana kinga na dawa. Tushirikiane tuangamize ugonjwa wa ukimwi kwani umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu.

41. Ni ugonjwa gani ambao hauwezi kusababishwa na uchafu?
A. Homa ya matumbo B. Malale
C. Kipindupindu D. Kuendesha

42. Ugonjwa hatari zaidi ni______
A. unaoua B. unaoambukiza
C. unaosambaa D. usio na tiba

43. Neno UKIMWI linamaanisha____
A. Ukosefu wa kinga mwingi
B. Upotevu wa kinga mwilini
C. Upungufu wa Kinga mwilini
D. Ukosefu wa kiini mwilini

44. Kulingana na mwandishi, maradhi ya _____
A. malaria hayastahili kumwua mtu
B. malaria huua kwa sababu ya ukosefu wa dawa
C. malaria huua watu wachache
D. malaria ni ugonjwa wa kuambukiza

45. Ni ugonjwa upi ambao huwaua watu wengi zaidi?
A. Ukimwi B. Kipindupindu
C. Malaria D Kifafa

46. Watu wengi huugua malaria msimu wa____
A. masika B. kiangazi
C. wowote D. joto

47. Malaria humwua mtu ikiwa____
A. ametibiwa hospitalini
B. hajapata matibabu mazuri
C. ametibiwa kwenye zahanati
D. ameumwa na mbu

48. Ni ipi si njia ya kujikinga malaria kulingana na habari hi?
A. Kudungwa sindano ya kinga
B. Kulala ndani ya chandarua
C. Kuharibu makao ya mbu
D. Kumeza vidonge ukienda sehemu zenye historia ya malaria

49. Mtoto wa mbu huitwa kiluwiluwi, naye mtoto wa nzi ni____
A. kiwavi B. kiluwiluwi
C. buu D. kiyoyo

50. Kichwa cha habari hii ni____
A. Ukimwi B. Tiba
C. Maradhi D. Kipindupindu